MWELEKEO WA KATIBA MPYA TANZANIA

Tulikotoka, Tulipo na Tuendako



JUKWAA LA KATIBA TANZANIA

policy forum

MWELEKEO WA KATIBA MPYA TANZANIA:
TULIKOTOKA, TULIPO NA TUENDAKO

Kimetayarishwa na: Jukwaa la Katiba Tanzania na Kikundi Kazi cha Serikali za Mitaa cha Policy Forum (LGWG)

Kimehaririwa na: Prof. Chriss Peter Maina

Kimefadhiliwa na: Policy Forum

Mchora Katuni: Simon Regis

Kimesanifiwa na Kupigwa Chapa na: Colourprint Ltd

Toleo la kwanza- Oktoba, 2016

ISBN: 978-9987-708-24-6

@ JUKATA/Policy Forum

Sehemu yoyote ya kitabu hiki inaweza kunakiliwa na kubadilishwa kukidhi mahitaji yanayotakiwa bila kuomba kibali ili mradi machapisho yake yatolewe bure. Machapisho yote ambayo ni ya kibiashara yatahitaji kibali kutoka JUKATA/ Policy Forum.

JUKATA/ Policy Forum watashukuru kupatiwa nakala ya chapisho lolote ambalo sehemu ya maandishi yake yamenukuliwa kutoka kitabu hiki

YALIYOMO

Dibaji ii

Vifupisho iv

1.0 Utangulizi 1

2.0 Katiba za Tanzania Hadi Sasa 1

3.0 Historia ya Mchakato wa Katiba Mpya 2

3.1 Rasimu ya Kwanza ya Katiba 4

3.2 Rasimu ya Pili ya Katiba Mpya 4

4.0 Bunge Maalum la Katiba 5

4.1 Mjadala Katika Bunge la Katiba 5

4.2 Kupitishwa Katiba Inayopendekezwa 7

5.0 Tulichojifunza 7

6.0 Mwelekeo wa Katiba Mpya Tanzania 8

6.1 Umuhimu wa Kuhuisha Sheria Zinazoongoza Mchakato wa Katiba Mpya 9

6.2 Mkutano Mkuu wa Kitaifa wa Katiba 12

6.3 Bunge Maalum la Katiba 14

6.4 Kamati ya Wataalamu 15

6.5 Kura ya Maoni ya Katiba 16

6.6 Mabadiliko ya Msingi Katika Katiba Mpya 17

6.7 Kipindi cha Mpito 18

7.0 Pendekezo la Ratiba ya Mwelekeo wa Katiba Mpya Tanzania Kuanzia 2016 Hadi 2020 20

8.0 Hitimisho 15

DIBAJI

Ndugu msomaji wetu na mtumiaji wa kitabu hiki tunakuletea kitabu hiki cha ***"Mwelekeo wa Katiba Mpya Tanzania: Tulikotoka, Tulipo na Tuendako"*** likiwa ni chapisho maalum katika awamu ya pili ya mchakato wa kuandika katiba mpya nchini Tanzania.

Kama ilivyokuwa kwenye kitabu chetu cha awamu ya kwanza, madhumuni ya kitabu hiki ni kujenga na kuongeza uelewa wa wa Tanzania juu ya katiba. Tofauti ya kitabu cha mwanzo kitabu hiki pia kinakusudia kutoa mapendekezo ya mwongozo wa namna ya kuendesha awamu ya pili ya kukamilisha zoezi hili la kitaifa la kuandika katiba mpya shirikishi ya wananchi.

Kitabu hiki pamoja na mambo mengine kitaibua masuala ambayo yameachwa kutoka kwenye Rasimu ya Katiba ambayo yanatakiwa yasisahaulike kwenye katiba inayopendekezwa kama alivyoyasemea Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alipopokea taarifa ya Uchaguzi Mkuu wa 2015 tarehe 23 Juni 2016 alipozindua rasmi awamu ya pili ya mchakato wa kukamilisha kuandika katiba mpya ya Tanzania.

Tunawashukuru sana wadau wetu JUKWAA LA KATIBA TANZANIA (JUKATA) ambao toka machapisho haya yalipoanza tumekuwa tukifanya kazi pamoja na hata sasa tumeendelea pamoja bila kuchoka wala kuachana njiani. Kipekee tunawashukuru waandishi wa kitabu hiki yaani Deus Kibamba na Hebron Mwakagenda ambao bila kuchoka tumekuwa nao pamoja. Mwisho tunawashukuru watu wote ambao wamekuwa wakitumia vitabu hivi kwenye mchakato toka mwanzo hata sasa na wengine wametupa mrejesho juu ya umuhimu wa kitabu hiki ambacho kimekuwa kama utabiri wa kitaalamu wa mchakato wa katiba Tanzania.

Kitabu hiki kitakuwa kifupi sana kwani historia ya mchakato ambayo ilikaa vizuri sana kwenye kitabu cha mwanzo hatutairudia tena kwenye kitabu hiki ila kwenye utangulizi tutaweka mambo yote yaliyofanywa kwenye awamu ya kwanza ya mchakato wa kuandika katiba mpya.

Tunatoa shukrani kwa wote walioshiriki kuandaa kitabu hiki kama ifuatavyo: Ndugu Israel Ilunde(YPC) kwa kuongoza kikosi kazi kuandaa kitabu hiki, wajumbe mahiri kwenye kikosi kazi akiwemo; Kellen Mngoya (HAFOTA), Regina Katabi (M-WACOD), Greysmo Mutashobya (HDT), Elinami John na Amne Islam (PF-Sekretarieti), Gotfried Sangana (CODEFA) na Mchereli Machumbana (JUKATA).

Semkae Kilonzo
Mratibu
Policy Forum

VIFUPISHO

APRM	African Peer Review Mechamism
AZAKI	Asasi za Kiraia
BMK	Bunge Maalum la Katiba
ECZ	Electoral Commission of Zambia
HDT	Health Promotion Trust
HOFOTA	Habitat Forum Tanzania
JUKATA	JUKWAA LA KATIBA TANZANIA
MMKK	Mkutano Mkuu wa Kitaifa wa Katiba
PF	Policy Forum
TMK	Tume ya Mabadiliko ya Katiba
UKAWA	Umoja wa Katiba ya Wananchi
YPC	Youth Partnership Countrywide

1.0 UTANGULIZI

Mchakato wa kuandika Katiba mpya kwa wa Tanzania ulianza kutokana na madai ya muda mrefu ya waTanzania kutaka Katiba Mpya itakayokidhi matakwa ya nchi ambamo wananchi ndio wenye kushika hatamu. Kitabu hiki kinaelezea jinsi mchakato wa kupata katiba mpya ya Tanzania ulivyoanza, ulipokwamia na jinsi gani ya kuendelea mbele ili kupata katiba mpya ya Tanzania.

Madhumuni ya kitabu hiki ni kuamsha mchakato wa Katiba Mpya ili kuukamilisha hadi kupata Katiba Mpya yenye muafaka wa kitaifa na kijamii. Nia ni kuhakikisha Tanzania inapata katiba yenye ubora na itakayokidhi matakwa ya wananchi. Kitabu hiki kinakusudia pia kutoa elimu, kuhamasisha na kushawishi upatikanaji wa katiba jumuishi yenye viwango vinavyokidhi. Mapendekezo, mafunzo na nini kifanyike vimeainishwa katika kitabu hiki kwa kuzingatia utashi chanya uliopo serikalini wa kuleta katiba mpya.

Kitabu hiki kimegawanyika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza inaeleza historia ya mchakato tangu ulipoanzishwa hadi ulipofikia. Sehemu ya pili inaelekeza tuendako na kupendekeza hatua na masuala muhimu ya kuzingatiwa katika kukamilisha mchakato. Kitabu kimerahisisha jinsi ya kuelewa namna mchakato mzima wa upatikanaji wa katiba ulivyoanza na ulipokwamia na ni nini cha kufanya. Malengo yetu ni kuwapa hamasa wananchi kudai katiba mpya ambayo itakuwa imejumuisha mawazo yao. Pia wafanya maamuzi wanachokozwa na kuhimizwa kuendelea au kuanzisha mchakato wa upatikanaji wa katiba mpya.

2.0 KATIBA ZA TANZANIA HADI SASA

Tanzania ni Jamhuri ya Muungano. Ni Muungano wa nchi mbili zilizoungana mnano tarehe 26 Aprili 1964, nchi hizi (Tanganyika na Zanzibar) awali zilikuwa huru na zenye mamlaka kamili. Katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zipo katiba mbili, katiba ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Hivyo, kwa upande wa Tanganyika na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumewahi kuwa na Katiba zifuatazo, katiba ya Uhuru ya Mwaka 1961, Katiba ya Jamhuri ya mwaka 1962, Katiba ya Tanzania ya Mwaka 1964 (Katiba ya Muungano), Katiba ya Muda ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1965 na Katiba ya Kudumu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Kwa kifupi, uandishi wa katiba zote tajwa hapo juu haukuwa shirikishi. Wananchi hawakupata nafasi ya kutoa maoni yao wakati wa mchakato wa kuandika katiba. Na pia, katiba zote ziliandikwa wakati Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa chini ya mfumo wa chama kimoja. Baada ya nchi kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi mwaka 1992, katiba ya Tanzania ya mwaka 1977 isingeweza kutumika bila kufanyiwa marekebisho makubwa. Kwa misingi hii, haja ya kuandika katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa haiepukiki.

3.0 HISTORIA YA MCHAKATO WA KATIBA MPYA

Mchakato wa uandishi na maudhui ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake 14 vimekuwa vikilalamikiwa kwa kutoshirikisha wananchi kikamilifu. Pamoja na mchakato kutokuwa shirikishi kwa wananchi, suala kwamba uandishi wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ulifanyika nchi ikiwa kwenye mfumo wa chama kimoja nalo limekuwa likilalamikiwa na wadau mbalimbali. Pia, mwaka 2010 Zanzibar ilipofanya marekebisho ya katiba yake ya mwaka 1984 ilipelekea madai ya kudai katiba mpya ya Muungano kuongezeka. Sambamba na hilo, hali ya kisiasa hasa wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 nayo ilidhihirisha haja ya kuandika katiba mpya ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza wakati na baada ya Uchaguzi.

Kwa kuzingatia hayo Rais wa awamu ya nne Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete katika hotuba ya kuuaga mwaka 2010 na kukaribisha mwaka 2011 aliridhia kuanza kwa mchakato wa upatikanaji wa katiba mpya. Pamoja na shinikizo la raia kupitia makundi yao mbalimbali hususani asasi za kiraia na vyama vya siasa, uamuzi wa Rais ulichochewa na zoezi la kujitathmini wenyewe tukiwa wanachama wa Mpango wa Kujitathmini Utawala Bora Afrika (APRM) tangu 2010.

Baada ya uwamuzi wa Rais, serikali iliandaa muswada na kuuchapisha katika Gazeti la Serikali mnamo tarehe 15 Machi 2011 na kuwasilishwa Bungeni Aprili 2011 ambapo baadaye ulipitishwa kuwa sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na. 8 ya mwaka 2011. Sheria hii iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhiwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984.

Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya 2011 ilimpa Rais mamlaka ya kuteua Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Rais aliteua Tume ya Mabadiliko ya Katiba ikiongozwa na Mwanasheria nguli, Jaji na Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Joseph Sinde Warioba ili kupata katiba ya kudumu miaka 50 hadi 100 bila haja ya kufanyiwa marekebisho makubwa. Makamu Mwenyekiti wa Tume alikuwa Mhe. Jaji Augustino Ramadhani, Jaji Mkuu Mstaafu wa Tanzania.

Wajumbe walioteuliwa walikuwa 32 (ikijumuisha Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti) wajumbe 16 kutoka Tanzania Bara na 16 kutoka Zanzibar. Muundo wa Tume ulihusisha wawakilishi wa vyama vya siasa, wasomi, AZAKI, madhehebu ya dini na makundi mengine katika jamii. Kulikuwa na sekretarieti kuiwezesha Tume kutekeleza majukumnu yake kwa ufanisi. Sekretarieti iliongozwa na Bw. Asaa Ahmad Rashid akiwa Katibu akisaidiana na Bw. Casmir Sumba Kyuki Naibu Katibu. Tume ilipewa miezi kati ya 18 na 20 ili kukusanya maoni na kuandaa rasimu ya katiba mpya.

3.1 RASIMU YA KWANZA YA KATIBA

Baada ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba kukusanya maoni kwa wananchi kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011, Tume iliandaa rasimu ya kwanza ya katiba ambayo kimsingi ilizingatia maoni huru ya wananchi. Kwa kutambua umuhimu na ushiriki hai wa wananchi kwenye uandishi wa katiba Tume iliirejesha rasimu hiyo kwenye Mabaraza ya katiba ya wananchi ili kuhakiki maoni yao na kuboresha zaidi pale ilipohitajika. Mabaraza ya Katiba ya wananchi yalifanya kazi kubwa ambayo iliendeleza msingi wa maoni ya wananchi waliyoyatoa kwenye hatua ya kukusanya maoni. Kutokana na maboresho yaliyotoka kwenye Mabaraza ya Katiba ya wananchi, Tume iliandaa rasimu ya pili ya katiba ambayo ilikabidhiwa kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete mnamo Disemba 2013.

3.2 RASIMU YA PILI YA KATIBA MPYA

Rasimu ya pili ya katiba kimsingi ilikuwa imejaa mambo mengi kama yalivyopendekezwa na wananchi kwenye hatua mbalimbali hadi kufikia kukamilika kwa rasimu ya pili ya katiba. Rasimu hii iliboresha zaidi masuala mazuri yaliyokuwemo kwenye rasimu ya kwanza. Iliweka bayana mgawanyo wa madaraka katika vyombo vikuu vya dola pamoja na kuwapa madaraka wananchi juu ya viongozi wao wanaowachagua wakati wa uchaguzi. Wananchi wengi waliipokea rasimu ya pili kwa hamasa kubwa sana wakiamini kuwa itakuwa mwanzo mzuri katika mchakato wa kuandika Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jambo ambalo lilionekana kuvuta hisia za wananchi wengi ni mapendekezo ya rasimu ya muundo wa serikali tatu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tofauti na ilivyo kwenye Katiba ya sasa. Rasimu ya pili ya katiba ndiyo iliyopelekwa kwenye Bunge Maalum la Katiba kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa kama katiba inayopendekezwa kuelekea kura ya maoni ili kupata katiba mpya.

4.0 BUNGE MAALUM LA KATIBA

Kwa mujibu wa Kifungu cha 22 (1) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Bunge Maalum la Katiba (BMK) lilikuwa na wajumbe kutoka makundi matatu. Kundi la kwanza lilikuwa ni wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kundi la pili lilikuwa ni wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Kundi la tatu lilihusisha uteuzi wa wajumbe 201 watakaoteuliwa na Mhe. Rais wa Muungano kutoka makundi mbalimbali ya kijamii hapa Tanzania. Makundi hayo ya kijamii yalikuwa ni AZAKI, taasisi za kidini, vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu, taasisi za elimu, makundi ya watu wenye ulemavu, vyama vya wafanyakazi, vyama vya wafugaji, vyama vya wavuvi, vyama vya wakulima na makundi mengine yenye malengo yanayofana. Makundi haya yote yalipewa idadi ya wajumbe kama sheria ilivyoelekeza.

Hata hivyo, uteuzi wa wajumbe hawa 201 ulilalamikiwa sana kutokana na sheria kumpatia Mhe. Rais mamlaka ya uteuzi wa mwisho kutokana na mapendekezo ya kundi husika. Wadau wengi walikosoa utaratibu huu kwa vile kimsingi uliwanyima wananchi madaraka yao ya uteuzi wa moja kwa moja. Na kwa mshangao, uteuzi wa wajumbe hawa 201 uliendeleza wimbi la kuwateua wanasiasa hata kwenye makundi ambayo kimsingi hawakupaswa kuteuliwa kama wajumbe wawakilishi wa hayo makundi. Uteuzi wa wajumbe wengi wanasiasa kwenye Bunge Maalum la Katiba ilikuwa ishara mbaya kwa maendeleo ya mchakato wa katiba.

4.1 MJADALA KATIKA BUNGE MAALUM LA KATIBA

Baada ya kuundwa na kuitishwa kwa BMK, Sheria ya Mabadiko ya Katiba ilielekeza kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kuwasilisha rasimu ya katiba ndani ya BMK baada ya kuzinduliwa rasmi na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, kutokana na hali ya kisiasa iliyokuwa hasa ikitokana na maudhui ya rasimu ya katiba, rasimu iliwasilishwa na Mwenyekiti

wa Tume kwenye BMK kabla ya uzinduzi kinyume na utaratibu ulivyokuwa.

Baada ya utaratibu kuwa umekiukwa na Mwenyekiti wa Tume kuwasilisha rasimu ya katiba kabla ya BMK kuzinduliwa, wakati akizindua BMK Mhe. Rais Kikwete alikosoa baadhi ya masuala hususan muundo wa muungano. Mhe. Rais Kikwete alitumia fursa hiyo ya uzinduzi wa BMK kukosoa vikali muundo wa serikali tatu uliokuwa umependekezwa na wananchi na kuingizwa kwenye rasimu ya katiba. Mhe. Rais Kikwete alieleza wazi msimamo wa chama chake kuwa unapinga muundo uliopendekezwa kwenye Rasimu. Hotuba ya Mhe. Rais Kikwete iliamsha hisia za wananchi, walikosoa hatua hiyo kwa vile alikuwa kinyume na utaratibu.

Tangu hapo, mijadala ya BMK ilitawaliwa zaidi na wanasiasa kuliko wajumbe waliowakilisha makundi mengine hususan kuweka mbele maslahi ya vyama. Hali hiyo ilisababisha mivutano na kutoelewana hatimaye idadi kubwa ya wabunge wa upinzani pamoja na baadhi ya wawakilishi wa wajumbe wa asasi kususia bunge hilo. Wajumbe wengi waliosusia Bunge Maalum la Katiba waliunda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) kupinga utaratibu wa uendeshaji wa BMK ambao waliamini usingeweza kuleta katiba mpya ya wananchi. Hii ni kutokana pia na matumizi mabaya ya muda, BMK ilitumia zaidi ya siku sitini kutunga kanuni za kuendesha chombo hicho.

Kutokana na udhaifu katika uendeshaji wa Bunge Maalum la Katiba, ilipatikana katiba inayopendekezwa ambayo iliacha baadhi ya maoni ya wananchi. BMK iliongozwa na Ndugu Samuel Sitta ambaye pia ni Spika Mstaafu wa Bunge la Tanzania akiwa kama Mwenyekiti na ndugu Samia Suluhu kama Makamu Mwenyekiti ambaye kwa sasa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

4.2 KUPITISHWA KATIBA INAYOPENDEKEZWA

Pamoja na malalamiko juu ya uendeshwaji wa BMK, katiba inayopendekezwa ilipitishwa tarehe 2 Oktoba 2014 na kuzinduliwa tarehe 8 Oktoba 2014. Hata hivyo, upitishwaji wa katiba inayopendekezwa ili kupata theluthi mbili ya wajumbe wa pande zote mbili za muungano ulikumbwa na kasoro kadhaa zikiwemo ile ya watu kupiga kura wakiwa hospitalini na wengine wakiwa nje ya nchi kwa njia ya simu. Aidha mjumbe aliyefariki na mwingine aliyesusia walionekana katika orodha ya waliopiga kura na baadhi ya wajumbe wa Tanzania Bara kuonekana kupigia kura upande wa Zanzibar.

5.0 TULICHOJIFUNZA

Kutokana na mchakato tumejifunza mambo yafuatayo:

(1). Ili kuwa na matokeo mazuri ya mchakato wa katiba mpya inabidi kutenga muda wa kutosha. Ni vema kukumbuka kwamba mchakato wa katiba siyo kama mkondo wa maji ambayo hutiririka moja kwa moja.

(2). Ni vigumu kuendesha mchakato wa katiba tukikaribia Uchaguzi Mkuu. Ni changamoto zaidi kupiga kura ya maoni na kura ya uchaguzi kwa wakati mmoja au uliokaribiana.

(3). Inapaswa wabunge wa BMK kuchaguliwa na wananchi ili kuweka kipaumbele maslahi ya wananchi na wasiteuliwe kwenye nyazifa nyingine kwa muda maalum.

(4). Mchakato wa kuandika katiba mpya umewawezesha wananchi kuwa na uelewa mkubwa zaidi kwenye masuala ya umma.

(5). Mchakato wa kuandika katiba mpya umeamsha ari ya wananchi kushiriki kwenye michakato ya kisiasa. Hii imejidhihirisha kwenye idadi ya wapiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 iliyoongezeka kutoka Milioni 8 (2010) hadi Milioni 15 (2015).

Uzoefu huu tulioupata utusaidie katika kumalizia mchakato wa katiba mpya tukiwa tunajiepusha na kasoro zozote.

6.0 MWELEKEO WA KATIBA MPYA TANZANIA

Mchakato wa katiba ulilazimika kusimama baada ya kupitishwa kwa katiba inayopendekezwa ili kupisha Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba, 2015. Hii ilikuwa ni pamoja na kutumika kwa mfumo mpya wa kielektroniki wa uandikishaji wapiga kura hapa Tanzania. Tunaamini kwamba wa Tanzania bado wanayo kiu ya kuona mchakato unakamilika na kukidhi matarajio yao ya kupata katiba itakayodumu miaka 50 hadi 100 ijayo bila marekebisho makubwa kama ambavyo alitamani Rais mstaafu Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa kuanzisha mchakato.

Kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya kwanza ya kitabu hiki kuhusu tulikotoka ni kwamba mchakato wa katiba kwa kawaida una hatua kadhaa, mfano tangazo la kuanzisha mchakato, utungaji wa sheria za kusimamia mchakato, ukusanyaji wa maoni ya wananchi kupitia Tume, uhakiki wa maoni kupitia mabaraza ya katiba, Bunge Maalum la Katiba kupitisha rasimu na kura ya maoni ya wananchi wote.

Kufuatia madai ya muda mrefu ya wananchi, hatimaye Rais wa awamu ya tano Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli aliridhia kuendeleza mchakato wa Katiba mpya alipozungumza Jijini Dar es Salaam mnamo tarehe 23 Juni 2016 alipokuwa akipokea taarifa ya uchaguzi wa mwaka 2015 kutoka kwa Tume ya Uchaguzi. Alisema yafuatayo:

> … Mchakato wa Katiba ulifikia mahali pazuri sana … Haya mengine yatakapofikishwa serikalini tutayafanyia kazi na wakati tutakapokuwa tunafanyia kazi inawezekana yakajitokeza mengine ambayo yanaweza kuwa *added* katika huo mchakato. Katiba ni ya wa Tanzania lengo

> letu ni kuipeleka Tanzania mahali pazuri … hiyo ndiyo ahadi yangu …

Kwa maoni yetu, kauli hii ya Rais Magufuli ni ahadi na ndoto muhimu sana katika kukamilisha mchakato wa katiba mpya. Inawataka wadau mbalimbali wa mchakato huu watumie fursa hii kujitokeza kushiriki kikamilifu kwenye hatua zinazofuata.

Katika hilo, wadau mbalimbali wanao wajibu wa kuchangia jitihada za upatikanaji wa sheria na kanuni ambazo zitaweka utaratibu mzuri wa kuwawezesha wananchi wote bila kujali tofauti zao kushiriki kikamilifu kwenye mchakato. Ushiriki hai wa wadau utaepusha mchakato kutekwa na baadhi ya watu wenye maslahi binafsi.

Viongozi makini ambao wako ngazi mbalimbali kuanzia Rais hadi wale wanaoongoza na kusimamia shughuli za kila siku katika ngazi ya jamii watahakikisha wanasaidia mchakato uwe huru na usioegemea upande wowote ili kuimarisha muafaka wa kitaifa.

6.1 *UMUHIMU WA KUHUISHA SHERIA ZINAZOONGOZA MCHAKATO WA KATIBA MPYA*

Tangu kuanza kwake, mchakato huu wa katiba umeongozwa na sheria mbili kwa vipindi tofauti. Awali, mchakato ulikuwa ukiongozwa na sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na. 8 ya mwaka 2011 (pamoja na marekebisho yake) na baada ya kupitishwa kwa katiba inayopendekezwa, Sheria ya Kura ya Maoni ya mwaka 2013 ikaanza kutumika pia.

Hata hivyo, kwa sasa sheria hizi haziwezi kutumika tena kuongoza mchakato bila kufanyiwa marekebisho kwa sababu za msingi kuu mbili ambazo ni kupitwa na wakati pamoja na utata wa sheria hizo hasa sheria ya Kura ya Maoni.

Kwa vile Sheria ya Kura ya Maoni iliweka vipindi vya muda maalum ili jambo au hatua mahususi kuwa imekamilishwa kuelekea Kura

ya Maoni, muda uliopangiliwa kutekelezwa kwa hatua kadhaa haukufanyika kama sheria ilivyoelekeza. Kwa mfano, Kifungu cha 4 (1) kilielekeza kuwa '*Rais kwa kushauriana na Rais wa Zanzibar ndani ya siku 14 baada ya kupokea katiba inayopendekezwa atatakiwa kuwa ametoa agizo kwenye Gazeti la Serikali kuitaka Tume ya Uchaguzi kuitisha Kura ya Maoni kuhusu Katiba Inayopendekezwa'.*



Hivyo kufikia tarehe 22 Octoba 2014, Rais alipaswa kuwa ametekeleza matakwa ya kifungu husika hapo juu. Pia, Kifungu cha 4 (3), kilielekeza kuwa '*ndani ya siku saba baada ya kuchapishwa kwa katiba inayopendekezwa, Tume ya Uchaguzi itapaswa kuwa imetunga na kuchapisha swali la Kura ya Maoni*.

Hivyo, kwa lugha nyepesi, swali la kura ya maoni lilipaswa kuwa limeshatungwa na kuchapishwa kwenye *Gazeti la Serikali* kabla ya tarehe 22 Oktoba 2014.

Aidha, Kifungu cha 5 (1) kinaeleza kuwa *Tume ya Uchaguzi ndani ya siku kumi na nne baada ya kuchapisha swali la kura ya maoni kwenye Gazeti la Serikali ikionyesha yafuatayo; (a) muda wa kuelimisha jamii kuhusu kura ya maoni juu ya katiba inayopendekezwa, (b) siku ambayo kura ya maoni itatakiwa kufanyika, (c) muda wa kupiga kura ya maoni.* Hivyo, kwa matakwa ya Kifungu cha 5 (1), kufikia tarehe 5 Novemba 2014 Tume ya Uchaguzi ilipaswa kuwa imetekeleza matakwa ya kifungu hiki.

Kutokana na kupitwa na wakati kwa vifungu tajwa hapo juu na vingine vingi, Sheria ya Kura ya Maoni ya 2013 haiwezi kutumika bila kufanyiwa marekebisho kwa vile Kura ya Maoni haikufanyika kama iliyokuwa imepangwa awali. Ili sheria hizi ziendelee kutumika pale mchakato utakaporejewa, ni lazima zifanyiwe marekebisho ili kurekebisha vifungu vyenye utata na kuhuisha vifungu vilivyopitwa na wakati.

Kwa msisitizo wa pekee, marekebisho kwenye Sheria ya Mabadiliko ya Katiba yazingatie ushauri wa kuirejesha Tume ya Mabadiliko ya Katiba kama chombo cha kitaalam hadi pale mchakato utakapokamilika. Inapendekezwa pia kuwa kabla ya kufanyika kwa marekebisho ya sheria hizi ni vizuri pia wadau wakapata fursa ya kushiriki kutoa maoni kuhusu masuala ya kufanyiwa marekebisho ili kupandisha kiwango cha muafaka kinachoonekena kuwa chini mno tangu kupitishwa kwa katiba inayopendekezwa.

Sababu ya pili ikiwa ni utata wa baadhi ya vifungu ambavyo vimeonekana kuwa na mgogoro, hasa sheria ya Kura ya Maoni. Baadhi ya vifungu vyenye utata ama vinavyokinzana ni pamoja na Kifungu cha 4 na Kifungu cha 5 (1) (b) (c). Kifungu cha 4 kimetoa mamlaka kwa Mhe. Rais kutangaza *kipindi* cha kufanyika Kura ya Maoni, wakati Kifungu cha 5 (1) (b) (c) kikitoa mamlaka kwa Tume ya Uchaguzi kutangaza *tarehe* na *muda* kufanyika kwa Kura ya Maoni.

Kwa utata huu, tarehe 30 April 2015 iliyokuwa imepangwa kwa ajili ya Kura ya Maoni ilitangazwa na Mheshimiwa Rais wa awamu ya nne alipokuwa kwenye ziara za kiserikali nchini China. Tangazo la Mheshimiwa Rais lilipokelewa kwa hisia tofauti kwamba ameingilia majukumu ya Tume kwa mujibu kwa Kifungu cha 5 (1) (b) (c). Sababu nyingine, ni kupitwa kwa wakati kwa vifungu vingi katika sheria hizi hasa sheria ya Kura ya Maoni ya mwaka 2013. Katika utungwaji wa Sheria ya Kura ya Maoni, matumizi yake yalianza baada ya katiba inayopendekezwa kukabidhiwa kwa Mhe. Rais wa awamu ya nne.

Mhe. Rais wa awamu ya nne alikabidhiwa katiba inayopendekezwa na Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba tarehe 8 Oktoba 2014 mjini Dodoma, hivyo matumizi ya Sheria ya Kura ya Maoni yalianza, msingi wake ukiwa ni tarehe tajwa hapo juu.

6.2 MKUTANO MKUU WA KITAIFA WA KATIBA

Kutokana na hali halisi ya mchakato wa katiba ya kiwango kidogo cha muafaka baina ya kundi linalokubaliana na katiba inayopendekezwa na kundi linalokubali rasimu ya katiba, ipo haja ya kuitishwa kwa Mkutano Mkuu wa Kitaifa wa Katiba.

Kazi kubwa ya mkutano huu itakuwa kupandisha kiwango cha muafaka hasa kwenye masuala ambayo bado yanabishaniwa au yamekosa muafaka wa kitaifa na yana umuhimu wa kuingizwa kwenye katiba mpya. Pia, mkutano huu unaweza kupendekeza ama kukubaliana mambo ambayo yataingizwa kwenye marekebisho ya sheria zinazosimamia mchakato wa katiba mpya Tanzania.

Jambo la kuzingatia katika kuitishwa kwa mkutano huu ni uwakilishi mpana wa wananchi kwa kutoa fursa kwa wananchi wenyewe kuchagua wajumbe wa mkutano bila kuingiliwa na vyombo vya serikali au mamlaka zingine. Pia, uwakilishi wa vyama vya siasa ndani ya mkutano huu uwe sawia, kisiwepo chama chenye wajumbe

wengi kuliko vyama vingine. Usawa wa kijinsia uwe bayana kwa kuzingatia uwakilishi wa makundi yote katika jamii ya wa Tanzania. Swala la idadi ya wajumbe wa mkutano huu litategemea uwezo wa kifedha wa serikali, ila kwa mapendekezo ni vizuri wajumbe wake wawe kati ya 400 hadi 700 na mkutano unaweza kufanyika kwa kipindi kisichozidi wiki mbili.



Uzoefu duniani unaonyesha kuwa kwenye hali kama hii ya mchakato wa kuandika Katiba mpya, Mkutano Mkuu wa Kitaifa wa katiba unaweza kuwa jawabu la kupatikana kwa katiba mpya. Kwa mfano, uzoefu kutoka nchi ya Nigeria unathibitisha kuwa katiba mpya inaweza kuzaliwa kutoka kwenye Mkutano Mkuu wa Kitaifa wa Katiba. Nigeria baada ya kuingia kwenye mkwamo wa kuandika Katiba mpya, serikali ilikubaliana na wazo la kuitisha Mkutano Mkuu wa Kitaifa wa Katiba ili kutatua matatizo ambayo yalipelekea

mkwamo wa mchakato. Na kupitia Mkutano Mkuu huo wa katiba, Nigeria iliweza kupata katiba mpya. Tanzania inaweza pia kujifunza na kutumia mtindo huu ambao ulisaidia nchi ya Nigeria kupata katiba mpya.

6.3 BUNGE MAALUM LA KATIBA

Endapo Mkutano Mkuu wa Kitaifa wa Katiba utaitishwa, mkutano huo utakubaliana juu ya ni njia ipi itumike ili kufanikisha sehemu iliyosalia katika mchakato wa katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



Pamoja na njia nyingine, mkutano mkuu unaweza kupendekeza uitishwaji wa Bunge Maalum la Katiba (BMK). Bunge hili linaweza kukaa kwa siku chache ikilinganishwa na zile za awamu ya awali ya mnano mwaka 2014. Pia, kutokana na ukweli kwamba kazi kubwa

imeshafanyika, Bunge hili Maalum la Katiba, linaweza kuwa dogo tofauti na lile lilopita. Inapendekezwa wajumbe wa BMK wasizidi 300. Hata hivyo, ni muhimu muundo wake kuzingatia usawa katika uwakilishi mpana wa wananachi ambao uamuzi wao utakuwa wa mwisho. Aidha uwakilishi wa makundi mbalimbali kama Bunge utazingatia msingi kwamba si wabunge wote watakuwa wajumbe wa BMK. Inapendekezwa idadi ya wajumbe kutoka bunge wasizidi asilimia 30 Kwa kuzingatia uwiano wa pande zote mbili za muungano na uwakilishi wa vyama.

Ni katika Bunge hili mambo muhimu yaliyoachwa kwenye katiba inayopendekezwa yanaweza kujumuishwa na kufanya marekebisho mengine ya msingi yanayopendekezwa na wananchi kwa wakati huu.

6.4 KAMATI YA WATAALAMU

Kama ilivyoainishwa hapo awali, sheria inaweza kuelekeza kwamba hatua inayofuata itakuwa ni Kamati Maalum ya Wataalamu ili kukamilisha mchakato wa kuandika katiba mpya kabla ya kwenda kwenye hatua nyinginezo. Kwa kawaida, zao la Kamati Maalum hupelekwa kwa ajili ya kuridhiwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kitaifa wa Katiba au BMK. Kama ilivyo kwa Bunge Maalum la Katiba (BMK), Kamati Maalum ya watu kati ya 20 hadi 30 itapangiwa muda maalum usiozidi siku 60 ili kukamilisha kazi yake.

Kamati ya Wataalumu itakuwa na jukumu la kupitia katiba inayopendekezwa na na nyaraka nyingine zinazohusiana na kuainisha masuala muhimu yanayopaswa kuingizwa katika rasimu ya mwisho ya katiba inayopendekezwa.

Pamoja na uchambuzi wa nyaraka, kamati pia itatoa nafasi ya kuwashirikisha wananchi kwa kuwaalika kutoa maoni yatakayosaidia kuboresha Katiba Inayopendekezwa.

6.5 KURA YA MAONI YA KATIBA

Katika uandishi wa katiba, hatua ya kupiga kura ya maoni haiepukiki. Kwa kawaida, Kura hii huhusisha wananchi wote waliotimiza umri wa mtu mzima, ikimaanisha miaka 18 na zaidi. Kura hii ni moja ya njia ya wananchi kuhakiki na kuidhinisha kuwa maudhui yaliyomo katika rasimu ya mwisho ya katiba yanasadifu maoni waliyoyatoa wakati wote wa utoaji au ukusanyaji maoni.

Kwa hapa Tanzania, hatua ya kupiga kura ya maoni imetamkwa na kubainishwa katika Sheria ya Kura ya Maoni ya mwaka 2013 kama hatua ya mwisho kuelekea kupitishwa kwa Katiba. Kiutaratibu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepewa jukumu la kuandaa na kuratibu kura ya maoni kwa kutunga swali ambalo kwa kawaida huwataka wananchi waseme endapo wanaipitisha katiba inayopendekezwa kwa kura ya NDIYO au HAPANA.

Hata hivyo, kutokana na mkanganyiko uliojitokeza katika hatua ya Bunge Maalum la Katiba, taifa letu linaonekana kugawanyika katika makundi mawili. Kwanza, wapo wanaoamini kuwa katiba inayopendekezwa, ambayo ni zao la Bunge Maalum la Katiba, haina kiwango cha kutosha cha muafaka kinachoifanya iweze kuletwa mbele ya wananchi kuipigia kura ya NDIYO au HAPANA. Hii ni kutokana na maoni mengi ya msingi ya wananchi yalipuuzwa na kuachwa na Bunge Maalum la Katiba. Pili, wapo wanaoamini kuwa kutokana na upungufu huo wa kimuafaka ikilinganishwa na rasimu iliyotayarishwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba, swali la kura ya maoni linapaswa kuwauliza wa Tanzania endapo wanaiunga mkono RASIMU YA KATIBA au KATIBA INAYOPENDEKEZWA?

Kura ya maoni hupaswa kuwa shirikishi zaidi kuliko mchakato mwingine wa utungaji wa sheria za kawaida. Aidha, kwa kuwa Katiba ni Sheria Mama, wananchi wote hata wale ambao hawajaandikishwa katika Daftari la Wapiga Kura ili mradi wanaweza kuthibitisha uraia

wao, wanakuwa na sifa ya kupiga kura ya maoni. Mfano wa hivi karibuni wa jambo hili ni katika nchi ya Zambia ambako wananchi wa nchi hiyo waliruhusiwa kupiga kura ya maoni ya katiba hata kama hawakuwa wapiga kura halali kwa mujibu wa Tume ya Uchaguzi ya Zambia (Electoral Commission of Zambia - ECZ).

6.6 MABADILIKO YA MSINGI KATIKA KATIBA MPYA

Moja kati ya uwezekano endapo katiba inayopendekezwa itapitishwa katika kura ya maoni pasipo kutoa fursa ya kupandisha muafaka ni kuandaa pendekezo la orodha ya mambo ya msingi yanayopaswa kufanyiwa mabadiliko katika katiba inayopendekezwa hata baada ya kura ya maoni. Kimsingi, hii hufanyika katika mazingira kama yale ya katiba inayopendekezwa hapa Tanzania kusemekana kutobeba baadhi ya masuala ya msingi ambayo wananchi wanaona yana ulazima wa kuingizwa.

Kwa hali halisi iliyopo sasa, njia ya kufanya mabadiliko ya msingi kwenye katiba mpya inaweza kuwa ndiyo kimbilio la mwisho endapo njia nyingine zilizopendekezwa kupandisha kiwango cha muafaka katika Kitabu hiki zitakuwa zimeshindwa kutekelezwa. Katika hatua hii kutakuwa na orodha ya masuala yalisiyozidi kumi ambayo wa Tanzania wanadhani yakiingizwa katika katiba yatasaidia kuiboresha na kuifanya ikubalike zaidi na watu wengi kuliko hali ilivyo kabla yake. Muswada wa mabadiliko hayo unaweza kuandaliwa na Serikali kwa kuzingatia pendekezo la Kamati Maalum ya Wataalam ambapo muswada huo utapelekwa kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano kupitishwa.

Kwa bahati nzuri, pendekezo linalofanana na hili tayari limewahi kutolewa mwezi Agosti 2014 wakati vyama vya siasa vilipokutana na Rais wa awamu ya nne, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mjini Dodoma na kupendekeza marekebisho ya msingi ya Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977 kabla ya kufanyika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Kwa sababu hiyo, pendekezo hili linafahamika angalau miongoni mwa wanasiasa.

Jambo la msingi ni kwamba utekelezaji wake utapaswa kutanguliwa na elimu pana ya uraia na kufuatiwa na taratibu zote za Bunge kujadili na kupitisha miswada muhimu, ikiwemo kupokea maoni ya wananchi kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Kwingineko, utaratibu huu umewahi kutumika katika nchi ya Afrika Kusini katika hatua za mwisho za upitishaji wa katiba ya nchi hiyo mwaka 1996 na ni jambo linalowezekana hapa nchini pia.

6.7 KIPINDI CHA MPITO

Ni kawaida kwa michakato ya katiba mpya kupitia kipindi cha mpito kati ya muda inapopitishwa katiba mpya hadi utekelezaji wake. Kipindi hiki huwa ni mahsusi kwa ajili ya kuliweka taifa katika maandalizi ya kimifumo, kiutawala na kiutendaji kuanza kutekeleza

katiba mpya. Baadhi ya mambo muhimu wakati huu ni kuongeza uelewa wa wananchi juu ya hali itakavyokuwa baada ya kuanza utekelezaji wa katiba mpya na kutungwa kwa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya kusaidia katiba mpya kutekelezwa.

Katika nchi jirani ya Kenya, kipindi cha mpito kilichukua takribani miaka miwili kati ya kupitishwa kwa katiba mpya ya mwaka 2010 hadi kuanza utekelezaji wake. Wakati huo wa mpito, kulikuwa na Sheria zaidi ya 64 zilizotungwa na Bunge la Kenya kama sehemu ya utekelezaji wa katiba yao mpya. Aidha, kulikuwa na maandalizi ya kimfumo katika kutekeleza muundo mpya wa kiuongozi na kiutendaji kwa mujibu wa katiba mpya ikiwemo kuweka taratibu za uajiri wa majaji, uchaguzi wa wabunge na viongozi na watendaji katika mihimili yote ya dola. Inashauriwa kuwa Tanzania iwe katika kipindi cha mpito kwa miaka miwili tangu siku ya kupatikana kwa katiba mpya.

7.0 PENDEKEZO LA RATIBA MPYA YA MWELEKEO MPYA WA KATIBA MPYA TANZANIA KUANZIA 2016 HADI 2020

Kutokana na maoni yaliyopendekezwa katika hatua zote ambazo mchakato unaweza kupitia kuanzia sasa hadi kupatikana kwa katiba mpya, inapendekezwa kuwa ratiba yake ya utekelezaji iwe kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

SHUGHULI/TUKIO	2016	2017	2018	2019	2020
Ufufuaji wa mchakato wa katiba mpya kupitia tangazo la Rais	Oktoba				
Tangazo la kuanza kwa ukamilishaji mchakato wa katiba mpya katika Gazeti la Serikali	Oktoba				
Marekebisho ya sheria zinazoongoza mchakato wa Katiba	Novemba	Februari			
Kuundwa na kuanza kazi kwa Kamati Maalum ya Wataalamu		Julai – Septemba			
Mkutano Mkuu wa Kitaifa wa Katiba		Oktoba			
Bunge Maalum la Katiba kukutana tena kupitisha rasimu ya mwisho ya katiba inayopendekezwa		Oktoba			
Kura ya maoni/maamuzi ya katiba mpya			Februari		
Marudio ya kura ya maoni/ maamuzi endapo imepigiwa kura ya HAPANA			Mei		
Sherehe za kutangazwa na kuzindua katiba mpya			26 Aprili / 01 Julai		
Kutungwa kwa sheria na kuundwa kwa taasisi zote muhimu za kutekeleza katiba mpya			Julai		Juni
Kuanza kutumika kwa katiba mpya			Julai		

N.B: Uhamasishaji na uelimishaji wananchi juu ya mchakato na maudhui ya katiba mpya litakuwa zoezi endelevu wakati wote wa hatua za ukamilishaji wa mchakato huu.

8.0 HITIMISHO

Wa Tanzania wana nafasi ya kufanya uamuzi wa kuipigia kura ya ndiyo katiba ambayo wataona imebeba matarajio yao na yenye mfumo bora zaidi wa uongozi wa umma usio na shaka ya kutekwa kwa mamlaka yao. Raia makini wanaweza pia kuikataa katiba inayopendekezwa kwa kura ya HAPANA endapo itakuwa imebeba zaidi maslahi ya watawala kuliko wananchi.

Kwa hatua tulipo sasa, Tanzania haiwezi kuendelea hatua ya upigaji wa kura ya maoni pasipo juhudi za kupandisha kiwango cha muafaka kwanza. Kazi ya kupandisha kiwango cha muafaka inaweza kuwa kupitia moja au zaidi ya hatua kama: Kamati Maalum ya Wataalamu kuanisha masuala yaliyomo katika katiba inayopendekezwa na maudhui yaliyomo katika rasimu zilizotangulia, Mkutano Mkuu wa Kitaifa wa Katiba kupitisha maudhui ya mwisho ya katiba inayopendekezwa au Bunge Maalum la Katiba kuitishwa tena kupitisha mambo ambayo yalisahaulika katika hatua yake ya mwanzo mwaka 2014.

Ni matumaini ya Policy Forum na JUKWAA LA KATIBA TANZANIA kwamba kitabu hiki kitakuwa chenye manufaa katika kuonesha njia ya wapi kwa kuelekea kuanzia hapa tulipo na namna ya kufanya hivyo.

JUKWAA LA KATIBA TANZANIA

policy forum

POLICY FORUM
S.L.P 38486, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2780200/255 782317434
Baruapepe: info@policyforum.or.tz
Tovuti: www.policyforum.or.tz